# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
## CHUO CHA UALIMU TARIME

**MKOA WA MARA**

**Simu Na:** 0756205420/0769828593
0782996655/0763783223.
**Barua Pepe:** tarimetc@moe.go.tz.

S.L.P. 199
**TARIME.**
TANZANIA

**Kumb. Na.** CCU/TRM/MU/26/Vol.II/2026 Tarehe: 04/06/2026
Bw/Bi. ………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU NGAZI YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI, KATIKA FANI YA SANAA NA MICHEZO MWAKA WA MASOMO 2026/2027 KWA NJIA YA KAWAIDA (MIAKA 2) NA KWA NJIA YA MASAFA (MIAKA 3 HADI 4)**

**1. UTANGULIZI**

Napenda kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya ualimu ngazi ya stashahada ya ualimu katika fani ya sanaa na michezo. Ninakupongeza sana kwa kuchaguliwa. Unatakiwa kuwasili chuoni tarehe 13/07/2026 bila kuchelewa. Nasisitiza kuwa ukiripoti baada ya tarehe 27/06/2026 hutapokelewa. Kwa wale watakaosoma kwa njia ya masafa mnatakiwa kujisajili pia kwa tarehe hizo. Wasiliana na namba za simu zilizopo kwenye maelekezo haya utapata ufafanuzi zaidi.

**2. MAHALI CHUO KILIPO**

Chuo cha Ualimu Tarime kipo katika wilaya ya Tarime, Mkoa wa Mara. Ukipanda basi kutoka Mwanza au Musoma unaweza kushuka Buhemba au Tarime Mjini. Vituo vyote viwili ni jirani sana na chuo na nauli ya pikipiki ni Tshs. 2000/=, bajaji Tshs 1000 na tax Tshs 4,000/=

Kauli mbiu ya chuo ni: **"Kutoa Mwalimu Bora".** Mara baada ya kusoma barua hii, fanya maandalizi kikamilifu ili uweze kuripoti chuoni kwa wakati. Baada ya kuripoti na kutimiza masharti utasajiliwa na kupangiwa darasa /mkondo (stream). Kwa wale wa njia ya masafa utaelekezwa namna ya kujisajili kwa kuwasiliana na namba za msajili (**0769 828593, 0756205420)**

## 3. MAHITAJI YA CHUO KWA AJILI YA USAJILI

### A: UTHIBITISHO WA VYETI KWA WANAOSOMA KAWAIDA

Shughuli ya kwanza wakati wa kusajiliwa itakuwa ni kuhakikisha sifa za kitaaluma kutokana na vyeti utakavyowasilisha. Kwa hiyo ni lazima uoneshe vyeti vifuatavyo: -

(i) Kwa wale waliomaliza kidato cha sita mwaka 2026 waje chuoni na **original results slips** za mwaka huo. Kwa wale waliomaliza kidato cha sita kuanzia mwaka 2025 kurudi nyuma, waje na vyeti vyao halisi.

(ii) Kwa wale waliohitimu mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti 2026 waje na **original result slip** na waliomaliza chuo nyuma ya mwaka 2026, waje na vyeti vyao halisi.

(iii) Njoo na cheti cha kidato cha nne

(iv) Njoo na cheti cha kuzaliwa.

(v) Njoo na folder file 01 kwa ajili ya kutunzia nyaraka zako

### B. UTHIBITISHO WA VYETI KWA WANAOSOMA KWA NJIA YA MASAFA

a) Utawasilisha cheti cha kidato cha nne

b) Utawasilisha cheti cha kuzaliwa.

c) Utawasilisha cheti cha ualimu ngazi ya Astashahada.

### C: ADA KWA WANACHUO WOTE

(a) Ada ni Tshs. **450,000/=** kwa mwaka kwa wanachuo wote

(b) Ada hii inaweza kulipwa kwa mkupuo mmoja au Tshs. **225,000/=** kwa kila muhula unapoanza.

(c) Ada inalipwa kwa kutumia **control number** utakayopewa na Mhasibu wa Chuo mwenye namba **0755308808.** Kwa mawasiliano zaidi tumia namba za simu zilizopo kwenye fomu hii ya kujiunga.

(d) Hairuhusiwi kulipa ada kwa kulimbikiza yaani kidogo kidogo.

**N.B. Ada hii isilipwe kwenye akaunti inayoonekena kwenye hii fomu**

**C: 1 MICHANGO KWA WANACHUO WANAOSOMA KWA NJIA YA KAWAIDA (MIAKA 2)**

(a) Huduma ya kwanza **Tshs 10,000/=** kwa mwaka.

(b) Usajili, kitambulisho na leaving certificate **Tshs 20,000/=** inalipwa mara moja kwa mwaka wa kwanza tu.

(c) Serikali ya wanachuo **Tshs 5,000/=** kwa mwaka.

(d) Kukodisha godoro **Tshs 10,000/=** kwa mwaka.

(e) Ulinzi **Tshs 30,000/=** kwa mwaka.

(f) Ukarabati **Tshs 25,000/=** kwa mwaka.

(g) Usafi na mazingira **Tshs 20,000/=** kwa mwaka.

(h) Michezo **Tshs 30,000/=** kwa mwaka.

(i) Bima ya afya **Tshs 50,400/=** kwa mwaka ni **kwa wale ambao hawana bima.**

(j) Tshirt ya chuo **Tshs 15,000/=** (zinapatikana chuoni) hulipwa mara moja tu

- ❖ Jumla ya michango yote ni **Tshs 215,400/=**
- ❖ Michango ilipwe kupitia Akaunti Namba: **30401000008** yenye jina la **Tarime Teachers College** iliyopo katika Benki ya NMB Tarime. Tumia jina la mwanachuo unapolipia.

**C. 2 MICHANGO KWA WANACHUO WANAOSOMA KWA NJIA YA MASAFA (MIAKA 3 HADI 4)**

| | | |
|---|---|---|
| i. | Usajili na kitambulisho | 20,000 |
| ii. | Huduma ya kwanza | 10,000 |
| iii. | Serikali ya wanachuo | 5,000 |
| iv. | Ufuatiliaji na uendeshaji wa mafunzo | 40,000 |
| v. | Michezo | 30,000 |
| vi. | Vifaa vya usafi | 20,000 |
| **vii.** | Ukarabati | 25,000 |
| | **JUMLA YA MICHANGO NI** | **150,000/=** |

**D: SARE ZA WANACHUO WANAOSOMA KWA NJIA YA KAWAIDA**

**(a) WASICHANA**

(i) Mashati 2 rangi ya light blue mikono mirefu.

(ii) Neck - tai dark blue na nyeusi

(iii) Sketi ya dark blue moja na nyeusi moja - ziwe na rinda box bila mpasuo, ziwe na belt la nchi (2) ndefu mpaka chini.

(iv) Koti la suti dark blue na nyeusi

(v) Viatu - vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu vya kufunga kwa kamba jozi (2).

(vi) Socks – stocking nyeupe jozi (2).

(vii) Nywele - zisukwe mtindo wa utii wa roda kuanzia 5 – 8 au kunyoa nywele fupi, au kufunga kwa nyuma.

**(b) WAVULANA**

(i) Shati 2 rangi ya light blue yenye mikono mirefu

(ii) Tai ndefu ya dark blue na nyeusi (mvao uwe wa kawaida kukaribia kitovu

(iii) Suruali ya dark blue na nyeusi zisiyo bana na zivaliwe kawaida ukubwa wa miguu ni **inchi 18** (suruali ya mtepesho na **"modo"** ni marufuku kwa mwalimu).

(iv) Koti la suti dark blue na jeusi


(iv) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufungwa kwa kamba na soksi nyeusi au dark blue jozi mbili (2).


(v) Nywele fupi za kawaida (hairuhusiwi kunyoa kipara).

**(c) WASICHANA WA KIISLAMU**

Sare ya chuo ni dark blue na nyeusi katika sketi, na shati ni light blue. **(hijabu ifuate rangi ya sare ya chuo)**.

PICHA 1





**MUONEKANO WA SKETI NA SURUALI**

**E: MAELEKEZO YA SARE ZINGINE KWA WANACHUO WANAOISHI CHUONI**

(a) Njoo na mahitaji yafuatayo pamoja na maelekezo yote yaliyoainishwa hapo juu: -

- **WAVULANA**
  - (i) Truck suit rangi ya light blue na bukta jozi moja ya bluu.
  - (ii) Socks stoking jozi mbili za bluu.
  - (iii) Raba za michezo ukizingatia kuwa unasomea sanaa na michezo.
  - (iv) T shirt nyeupe za michezo za kuvaa ndani ya tracksuit

- **WASICHANA**
  - (i) Truck suit rangi ya light blue.
  - (ii) Sketi (**solo**) jozi mbili rangi ya light blue fupi kwa ajili ya michezo.
  - (iii) Viatu raba jozi mbili. Ni lazima kwani kozi yako ni sanaa na michezo.
  - (iv) Stoking jozi mbili.
  - (v) Tshirt nyeupe za kuwalia ndani ya tracksuit

**F: MAHITAJI KWA AJILI YA MALAZI NA MAZINGIRA**

- Chuo kinakodisha magodoro kwa watakaowahi. Endapo mwanachuo atachelewa kuripoti na kukosa godoro atalazimika kununua godoro lake.
- Shuka mbili (2): Moja ya rangi ya pinki na nyingine ya rangi bluu.
- Blanketi kwasababu ni mazingira ya baridi japo sio kali sana.
- Neti nyeupe ya kujikinga na mbu kwasababu huku kuna mbu
- Ndoo ya lita 20, bakuli, sahani, kikombe na kijiko.
- Wasichana waje na squeezer moja kwa ajili ya kusafisha eneo lako, na wavulana reki yenye mpini kwa ajili ya usafi wa kiunga utakalopewa.

**G: MAHITAJI YA LAZIMA KWA AJILI YA TAALUMA**

- Madaftari yasiyopungua 12 makubwa (quire 2 au 3).
- Kalamu za kutosha kwa ajili ya kuandikia (bluu au nyeusi).
- Ream moja (01) ya karatasi za A4 aina ya **Double A.**
- Ada ya mtihani wa Taifa **Tshs 50,000/= (**hii italipwa mara moja kwa miaka yote ya mafunzo).

- Picha mbili za passport size za hivi karibu.

4. **ZINGATIA PIA YAFUATAYO**
   - (i) Chuo hakitoi chakula maalumu (special diet kwa wenye changamoto binafsi).
   - (ii) Pima afya yako kikamilifu kabla ya kuja chuoni. (**katika hospitali ya serikali**)
   - (iii) Ikibainika kuwa cheti chako cha taaluma kimepatikana kwa udanganyifu hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yako.

**NB:** Wanachuo watakaosoma kwa njia ya masafa hawatakuwa na sare maalumu. Kutakuwa na nyakati za kukutana ana kwa ana chuoni na kuna wakati njia ya kielektroniki itatumika. Hivyo maelekezo mengine mtayapata wakati mkiendelea na mafunzo kwa njia ya masafa. Kwa mawasiliano zaidi piga namba za simu zifuatazo: **0769 828593, 0756205420, 0783173397** au **0763783223.**

Karibu Sana Chuo cha Ualimu Tarime.

ROMAN M. URASSA
**MKUU WA CHUO**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU TARIME
S.L.P. 199 TARIME-MARA

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
GOVERNMENT OF TANZANIA

**PART A: 3**

**From:** Principal,
Tarime Teachers College,
P.O. Box 199,
**TARIME.**

To: Medical Officer,
…………………………………..
…………………………………..
…………………………………..

Mr. /Mrs./Miss……………………………………………………………………………….
(Name in -Full)

Please examine the above named as his/her physical and mental fitness for a full time Teacher Training Course. The examination should include the following categories (I-III) each category of which will render the applicant ineligible in case of defect. Pregnancy (category IV) will render a girl's candidate ineligible for the course.

A:1 a) Eye Sight
b) hearing
c) Speech
d) Venereal diseases
e) Leprosy
f) Limbs
g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other serious diseases
4. Pregnancy
5. Ulcers
B: Blood Group

Yours faithfully,

ROMAN M. URASSA
**MKUU WA CHUO**
MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU TARIME
S.L.P. 199 TARIME-MARA

## PART B: MEDICAL CERTIFICATE
**To be completed by a Government Medical Officer**

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for a fulltime Teachers Training Course.

I a) Eye Sight…………………………………

b) hearing ………………………………….

c) Speech…………………………………..

d) Venereal diseases……………………….

e) Leprosy………………………………….

f) Limbs……………………………………

g) Epilepsy…………………………………

II. Neuroses…………………………………………

III. Other serious diseases……………………………….

IV. Pregnancy……………………………………………

V. Ulcers…………………………………………………

B: Blood Group…………………………………………

Name ……………………………………………………. Designation……………………………..….

Signature …………………………………………….……. Date ………….……………………………

Official Stamp